



Taarifa kwa Umma, Jumatatu, 27 Aprili 2011

Hatua kali zichukuliwe dhidi watumishi wa afya wanaojihusisha na rushwa!

Serikali ichukue hatua kali dhidi ya watumishi wa afya wanaohibitika kujihusisha na vitendo vya rushwa wakati huohuo wananchi wasifumbie macho matukio ya rushwa kama tuna nia ya dhati ya kuondoa tatizo la rushwa katika vituo vya afya.

Hivi karibuni, vyombo vya habari vimeripoti kwamba, mkunga katika hospitali ya Temeke alikataa kumhudumia mama mjamzito kwa sababu tu mama huyo alikataa kumpa mkunga huyo pesa ya chai (Tsh 4,000). Mkunga huyo alidai kwamba pesa hiyo ilikuwa ni kwa ajili ya kununulia vifaa muhimu vya kujifungulia ingawa mjamzito huyo aliweka wazi kwamba alikwenda hospitalini akiwa na vifaa vyake vya kujifungulia. Tukio kama hilo pia limeripotiwa kutokea katika wilaya ya Kahama ambako Sebonia Faustin (22) alitoa taarifa kwamba mtoto wake alifariki mara tu baada ya kuzaliwa kwa sababu alikataa kuwapa wakunga wa zamu Tsh 2,000 walioitaka walipwe ili wamuhudumie mtoto huyo.

Sikika imeguswa na matukio hayo, kwani pamoja na kuwepo kwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (PCCB), hongo na aina nyingine za rushwa zimeendelea kukithiri hapa nchini na hakuna mipango madhubuti ya kutokomeza tatizo hili linaloathiri sana wananchi wenye kipato cha chini. Kukithiri kwa matukio haya ya rushwa katika vituo vya kutolea huduma za afya kunadhihirisha wazi kushindwa kwa hatua ambazo Serikali imekua ikizichukua kudhibiti vitendo hivyo ikiwa ni pamoja na kuwahamisha au kuwashusha vyeo wafanyakazi wa afya ambao wanajihusisha na rushwa.

Uwepo wa rushwa ndogondogo katika huduma za afya, unawanyima wananchi haki yao ya kutumia huduma za afya hususani wenye kipato cha chini na inarudisha nyuma juhudi za nchi yetu katika kufikia Malengo ya Millenia (MDGs) hasa lengo namba 4 na 5 ambayo yamedhamiria kupunguza vifo vya wanawake na watoto ifikapo mwaka 2015.

Sikika inasikitishwa na tabia za baadhi ya wafanyakazi wa afya kushindwa kutekeleza sera ya serikali juu ya huduma za bure za afya kwa wanawake wajawazito na kutokuzingatia maadili ya kazi zao. Ili kutathmini hali ya wa matukio ya rushwa katika vituo vya huduma za afya katika mikoa ya Dar es Salaam na Mkoa wa Pwani, Sikika, ilifanya utafiti kuhusu rushwa ndogondogo katika huduma za afya ambao ulidhihirisha kuwa asilimia 55 ya wagonjwa wamekuwa wakiombwa rushwa katika kila kituo kituo cha afya walichohudhuria.

Hivyo, Serikali inapaswa kuchukua hatua kali zaidi dhidi wafanyakazi wa afya wanaojihusisha na vitendo vya rushwa kwani kuwahamisha au hata kuwashusha vyeo kama inavyofanyika sasa ni sawa na kuhamisha na kuongeza tatizo hilo.

Sikika pia inaamini kwamba ni jukumu la kila mwananchi kupambana na vitendo vya rushwa. Pia, ni wajibu wa Wananchi kuchukua hatua dhidi ya wafanyakazi husika, si tu kukataa kulipa hongo lakini pia kutoa taarifa juu ya wafanyakazi wanajihusisha na vitendo vya rushwa kwa wakuu wao wa kazi na vyombo vya dola.

Mr. Irenei Kiria